

WIZARA YA AFYA

MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO



JARIDA LA MTANDAONI

TOLEO NO. 2

SEPTEMBER - DESEMBER 2020

MARUFUKU WANAFUNZI KUPEWA VIDONGE VYA 'FOLIC ACID' SHULENI - WAZIRI UMMY

NA EMMANUEL MALEGI-MOROGORO

Shule zote nchini zimepigwa marufuku kuwapa wanafunzi (wasichana balehe) dawa aina ya Folic Acid badala yake zimesisitizwa kuhakikisha zinawajengea uwezo wa kulima maboga na mbogamboga katika bustani zao.

SOMA ZAIDI UK. 4



NHIF wezesheni wananchi wengi zaidi kujiunga na huduma - Serikali

SOMA ZAIDI UK. 4



SIMAMIENI USAJILI WA DAWA ZA ASILI, WAPENI ELIMU YA KUTOSHA WATENGENEZAJI - PROF. MCHEMBE

SOMA UK. 14

HATUNA uhaba wa chanjo nchini - Dkt. subi

SERIKALI kusaini Hati ya Sh. Bil 125.69 kuimarisha huduma za afya ngazi ya msingi

WAPEWA miezi sita kuongeza kasi katika kupunguza vifo vya mama na mtoto

WAUGUZI na Wakunga wasiohuisha leseni zao kuchukuliwa hatua

MWENYEKITI:
Prof. Mabula D. Mcembe
Katibu Mkuu

WAJUMBE:
Prof. Abel Makubi
Mganga Mkuu wa Serikali
Gerard Chami
Mkuu wa Kitengo Mawasiliano ya Serikali

MHARIRI:
Catherine Sungura

WACHANGIAJI:
Catherine Sungura
Englibert Kayombo
Emmanuel Malegi
Rayson Mwaisemba

MAWASILIANO:
Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii,
Jinsia, Wazee na Watoto
Mji wa Serikali Mtumba, Barabara ya Afya
S.L.P 743
40479 DODOMA.
Simu: +255 26 232 3267

JARIDA HILI LINATOLEWA NA
KITENGO CHA MAWASILIANO YA
SERIKALI-IDARA KUU AFYA

#tumeboreshaafya



Wauguzi na Wakunga tumieni utaalamu wenu kwa Ustawi wa Taifa

Miongoni mwa kada muhimu katika sekta ya afya ni hii ya wauguzi na wakunga ambayo kwa sehemu kubwa watoa huduma wake huwa karibu zaidi na jamii (wagonjwa) na ndio mtu wa kwanza kwa wagonjwa wanapofika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Ili kufikia malengo na matumaini ya wateja kada hii ni lazima isimamie na kutoa huduma kwa kuzingatia miongozo iliyopo kwa weledi mkubwa na kwa kutumia utaalamu wao ipasavyo kwa ajili ya ustawi wa Taifa letu.

Wauguzi na wakunga ndio watendaji wakuu katika vituo vya afya kwenye ngazi ya jamii hadi Taifa hivyo kuwajibika na utawala bora utaboresha utendaji pia kuhakikisha kufikia malengo mbalimbali walijoyiwekea katika ngazi zote.

Viongozi wanatakiwa kuwa wabunifu, wachapa kazi, wenyewe nidhamu na mfano bora wa kuiwga katika utekelezaji wa majukumu yenu, kwahiyoo ni lazima msimamie utoaji wa huduma uliyo mzuri na wenyewe heshima na utu.

Aidha,
nawakumbusha
kuwa katika
huduma za Uuguzi

na Ukunga ni ubinadamu zaidi na hivyo kuvaa viatu vya wagonjwa wenu. Hakuna aliyegongwa muhuri wa kuugua au kuwa mgonjwa akalazwa, "sisi sote ni wagonjwa watarajija kwa hiyo kama ambavyo sisi tungependa kuuguzwa vizuri, kujibiwa kwa kauli nzuri basi tuhakikishe tunasimamia maadaili ya kazi".

Serikali inawahakikisha itaendelea kufanya kazi pamoja na wauguzi kwa kutoa miongozo thabitii na kuhakikisha upatikanaji wa nyenzo muhimu katika hospitali na vituo vya kutolea huduma ya afya na kuboresha mazingira ya kazi yaliyo bora na salama.

Hivi karibuni kumekuwa na malalamko mbalimbali ya kiutendaji na kitaaluma kutoka kwa wateja wanaofika kupata huduma za kiafya na hivyo kuleta taswira mbaya kwa taaluma yenu na kuonyesha hakuna usimamizi mzuri wa utoaji huduma za uuguzi na ukunga.

Tungependa wateja wetu watoe sifa badala ya malalamiko hivyo mnapaswa kuwa na mipango ya kuondokana na malalamiko kwani taaluma yenu ni zaidi taaluma.

Kuhusu suala ya rushwa mnatakiwa kuwa mstari wa mbele kupambana na rushwa na kuhakikisha inatokomezwa katika maeneo yenu ya kazi kwani rushwa imekuwa ikilalamikiwa na kuriptiwa katika kada ya afya nchini.

**PROF. MABULA D. MCHEMBE
KATIBU MKUU-AFYA**



#tumeboreshaafya

Marufuku wanafunzi kupewa vidonge vyatya 'folic acid' shulen - Waziri Ummy

NA EMMANUEL MALEGI-MOROGORO

Shule zote nchini zimepigwa marufuku kuwapa wanafunzi (wasichana balehe) dawa aina ya Folic Acid badala yake zimesisitizwa kuhakikisha zinawajengea uwemo wa kulima maboga na mbogamboga katika bustani zao.

Agizo hilo lilitolewa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu alipokuwa akihitimisha kilele cha Maonesho ya Nanenane Kanda ya Mashariki inayojumuisha Mikoa ya Dar Es Salaam, Pwani, Tanga na Morogoro ambayo yalifanyika Mkoani Morogoro.

Waziri Ummy alisema ni marufuku kuwapa wanafunzi na wasichana balehe vidonge hivyo na kwamba fedha zinazotolewa kwa ajili ya kununua dawa hizo zitumike kuanzisha bustani shulen ili kuzalisha vyakula vinavyotoa madini hayo.

"Mbali na kuanzishwa kwa bustani shulen lakini pia fedha

hizo zinaweza kupelekwa kwa vijana ili waanzishe miradi ya bustani za mboga kwa ajili ya kuzalisha mazao yanayozalisha asidi hiyo yakiwemo maboga, matunda na hata karoti badala ya kutoa vidonge kwa wanafunzi," alisema Ummy.

Pamoja na hayo, Waziri Ummy alisema utafiti wa Shirika la Afya Duniani (WHO) unaonesha kila mtu anatakiwa kunywa nusu lita ya maziwa sawa na lita 180 kwa mwaka, lakini kwa sasa kila mtu anakunywa lita 40 kwa mwaka sawa na vijiko 10 vya chai kwa siku.

Akizungumzia hali ya udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano nchini, alisema umepungua kutoka asilimia 34.4 mwaka 2014 hadi asilimia 31.8 mwaka 2018 licha ya kuwa jitihada zinatakiwa kuendelea kuchukuliwa.

Aidha, aliupongea Mkoaa wa Morogoro kwa kuwa mwenyeji wa maonesho hayo ambayo yamekuwa chachu ya ukuaji wa kilimo, uvuvi na ufugaji pamoja na ujasiriamali nchini.

Aliwataka waratibu wake kutoisha hapo na badala yake ujuzi huo upelekwe vijijini

kwa ajili ya kuendeleza sekta hiyo muhimu ambayo kwa kiasi kikubwa inachangia pato la taifa.



NHIF wezesheni wananchi wengi zaidi kujiunga na huduma- Serikali

NA ENGLIBERT KAYOMBO, MOROGORO

Menejimenti ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), imeagizwa kubuni na kutekeleza mikakati ya kuwawezesha wananchi wengi zaidi kujiunga na kunufaika na Mfuko huo ili kufikia adhma ya Serikali ya Afya Bora kwa wote (UHC).

Wakati huo huo, Serikali imezionya hospitali zote nchini kuacha mara moja kufanya udanganyifu katika mada

ya malipo yatokanayo na huduma wanazozitoa kwa wanachama wa NHIF.

Yalielezwu hayo na Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dkt. Godwin Mollel alipozungumza na Menejimenti ya NHIF na waandishi wa habari mjini Morogoro kuhusiana na uboreshaji wa huduma za NHIF kwa wanachama na wananchi kwa ujumla.

"Nawapongea mmeweka utaratibu wa kila mwananchi kuweza kujiunga

lakini ongezeni jitihada katika kuwafikia wananchi kule waliko ili waweze kujiunga, wawe na uhakika wa kupata huduma za matibabu, Serikali itaendelea kuulea Mfuko huu ili uimarie na kuendelea kupanua wigo na ubora wa huduma kwa wananchi wote, hivyo natoa onyo kwa vituo vinavyojihusisha na udhanganyifu wowote," alisema Dkt. Mollel.

Alisema kuwa Serikali imeneedelea kuweza mikakati mbalimbali ya kuboresha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wananchi ikiwamo kuongeza bajeti ya dawa kutoaka bilioni 30 mwaka 2015 hadi kufikia bilioni 270.

"Tumeona uboreshaji wa miundombinu ya huduma za hospitali ikiwemo ujenzi wa zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya na hospitali za rufaa za mkoa, kuongeza madaktari katika vituo vya kutolea huduma za afya ngazi za chini na kuongeza vituo tiba na vitendanishi ili kuwezesha wananchi wengi kupata huduma karibu na maeneo wanayoishi, haya ni mafanikio makubwa" alisema Naibu Waziri.

Alisema kwa kutambua umuhimu wa Bima ya Afya kwa Wananchi na

huduma zitolewazo na Bohari Kuu ya Dawa (MSD), Serikali kuitia Wizara ya Afya, imekutana na Viongozi waandamizi wa NHIF na MSD kwa lengo la kupanga mikakati ya utatuza wa changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo.

Kutokana na kikao hicho, Serikali imefanya maboresho katika orodha ya Taifa ya Dawa muhimu kwa kuongeza aina ya dawa 71 ambazo hazikuwepo awali ambapo NHIF tayari umeongea dawa hizo katika kitita chake cha mafao kitolewacho kwa wanufaika wake.

"Tumeielekeza NHIF kuwasilisha maboresho ya kitita cha huduma zitolewazo kwa wanachama kwa ajili ya maamuzi na kuanza kutumika, kufanya mapitio ya utaratibu wa mikopo itolewayo kwa watoa huduma ikiwemo ya dawa, ukarabati wa vituo, vifaa tiba na vitendanishi ili kuongeza tija na kupunguza gharama," alisema.

Katika kikao hicho, Naibu Waziri huyo aliongozana na Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Abel Makubi na Mkurugenzi Mkuu wa MSD,

Brig. Jen. Dkt. Gabriel Sauli Mhidize.



Serikali kusaini Hati ya Sh. Bilioni 125.69 kuimarisha huduma za afya ngazi ya msingi

NA CATHERINE SUNGURA, WAMJW-DODOMA

Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendelo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo wanaochangia sekta ya afya kupitia Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund) imeridhia kuweka saini Hati ya Shilingi Bilioni 125.69 kwa ajili ya kuimarisha huduma za afya katika ngazi ya msingi nchini.

Akiongea wakati wa kuidhinisha makubaliano hayo, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Prof. Mabula Mchembe alisema lengo kuu la Mfuko huo tangu ulipoanzishwa mwaka 1999 ni kuimarisha huduma za afya katika ngazi ya msingi (halmashauri) zote nchini.

Alisema katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2020/21 Wadau nane (8) watachangia jumla ya USD 53.84 sawa na Shilingi bilioni 125.69 kwa kipaumbele cha kuimarisha huduma za afya katika vituo vya afya kwenye halmashauri zote 184 nchini.

"Shilingi bilioni 105.32 zitatumika kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa huduma za afya katika vituo vya afya vipatavyo 5,533 kwenye halmashauri zote 184 ikiwa ni pamoja na ununuzi wa dawa, vifaa na vifaa tiba, uendeshaji wa vituo, ukarabati mdogo na huduma za chanjo na vikoba.

"Fedha hizo zitapelekwa


moja kwa moja vituoni kwa utaratibu wa 'Direct Health Facility financing,' afafanua Prof. Mchembe.

Aidha, Prof Mchembe alisema Shilingi bilioni 4.29 zitatumika kuziwezesha Timu za Afya za Mikoa 26 kufanya ufuatiliaji na usimamizi shirikishi katika halmashauri zote nchini na Shilingi bilioni 2.09 zitawezesha Ofisi ya Rais - TAMISEMI kusimamia na kutoa msaada wa kitalaam katika halmashauri na mikoa yote nchini.

Aliongeza kuwa Shilingi bilioni 5.13 zitawezesha Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kutekeleza masuala ya sera, mikakati na miongozo kwa ajili ya kuhakikisha huduma za afya zinatolewa kwa kiwango na ubora stahiki na Shilingi bilioni 8.86 zitakuwa kwa ajili ya kutekeleza maeneo mengine ya kipaumbele katika sekta.

"Vipaumbele tulivyoihinsha na kamati ni pamoja na kutoa mafunzo kwa watalaam 620 wa dawa za usingizi, kununua machine za kisasa za kutolea dawa za usingizi katika vituo vya afya ngazi ya halmashauri na kufanya ukarabati mkubwa katika vyuo vinne vya kutolea mafunzo ya watalaam wa afya," alisema.

Prof. Mchembe alitaja maeneo mengine ya kipaumbele yaliyoihinsha na Kamati Kuu ya Mfuko huo ni kuhuisha Mkataba wa



Makubaliano (MOU) baina ya pande zote mbili kwa kipindi cha 2021 - 2026, kununua mashine za kutolea dawa za usingizi katika vituo vya afya kipamoja na kuvijengea uwezo vituo vya afya katika kusimamia na kutumia fedha kwa kuzingatia miongozo na taratibu mbalimbali.

Maazimio ya uwekaji saini Hati hiyo yamefanyika kwenye ofisi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya

Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto iliyoko mji wa Serikali Mtumba.

Hafla hiyo imehudhuriwa na watalaam wa Wizara hiyo na wengine kutoka Wizará ya Fedha na Mipango, OR - TAMISEMI, Bohari ya Dawa na Wadau wa Maendeleo wanaochangia Mfuko huo kutoka Canada, Denmark, KOICA, Ireland, Switzerland UNICEF, UNFPA na Benki ya Dunia ambao wameshiriki kwa njia ya 'video conference'.

Wauguzi wasisitizwa kufuata maadili wanapotoa huduma

NA EMMANUEL MALEGI-DODOMA

Mkurugenzi wa huduma za Uuguzi na Ukunga kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Bi. Ziada Sellah, aliwatembelea Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma ili kujionea hali ya utoaji wa huduma za afya pamoja kuona mazingira ya kazi hususani kwa wauguzi wa hospitali hiyo.

Mkurugenzi huyo licha ya kutembelea maeneo mbalimbali ya hospitali hiyo pia alizungumza na kusikiliza kero zinazowakabili

wauguzi hao ikiwemo kutopandishwa madaraja kwa wakati, upungufu wa vitendeza kazi kama kuwepo kwa mashuka machache ambayo hayakidhi idadi ya vitanda vilivyopo nakadhalika.

Pamoja na kuahidi kushughulikia kero hizo, Bi. Ziada aliwasisitiza wauguzi hao kuzingatia maadili wakiwa maeneo ya kazi na kuwataka kujiendeleza kimasomo ikiwa ni pamoja na kufanya tafiti ndogo ndogo zitakazowasaidia kufanya vyema katika taaluma yao.



MATUKIO MBALIMBALI KATIKA KIKAO CHA WIZARA NA VYUO VIKUU VYA AFYA KUHUSU UZALISHAJI WA RASILIMALI WATU WA SEKTA YA AFYA



Hatuna uhaba wa chanjo nchini - Dkt. Subi

NA CATHERINE SUNGURA - DODOMA

Serikali kuititia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imesema haina upungufu wa chanjo ya aina yeyote na kuwataka wazazi/walezi kuwapeleka watoto wao kuwapatia chanjo kulingana na ratiba zao, kwene vituo vya kutolea huduma za afya.

Mkurugenzi wa Kinga wa Wizara, Dkt. Leonard Subi alisema hayo wakati alipotembelea ghala ya kuhifadhi chanjo iliyopo hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma kukagua hali ya chanjo katika mkoa huo.

Dkt. Subi alisema chanjo zote aina tisa ambazo zinakinga dhidi ya magonjwa kumi na tatu zipo kwene ghala hilo.

"Tulikua na upungufu wa aina mbili za chanjo nchini kati ya tisa ambazo tumekuwa tukizitoa lakini, sasa hivi chanjo zote zipo, kwani zimeshawasili na usambazaji unaendelea," alisitisiza Dkt. Subi.

Hata hivyo Dkt. Subi alifanua upungufu huo wa chanjo ultokea baada ya Dunia kukumbwa na janga la mlipuko wa ugonjwa wa homa

kali ya mapafu (COVID-19) ambapo anga zote zilifungwa, utaratibu ni kwamba chanjo husafirishwa kwa mnyororo baridi, kwa hiyo huitaji usafiri wa anga.

"Chanjo sasa zimeanza kuingia nchini, hadi sasa mikoa 13 chanjo hizi zimeshapokelewa kati ya mikoa 26 na mikoa mingine kumi na tatu ya Tanzania Bara usambazaji unaendelea kuititia Bohari ya Dawa (MSD)," alisema.

"Waganga Wakuu wa Mikoa na Halmashauri wote nchini hakikisheni chanjo hizo mnazipeleka kwene vituo vyetu vya kutolea huduma za afya na muwajulise wananchi kwamba chanjo zipo na zinapatikana bila malipo yeyote, wazazi na walezi pelekeni watoto wenu kupata chanjo katika mikoa yenu," alisitisiza Dkt. Subi.

Aidha, aliweka bayana kwamba chanjo zilizopungua kwa mwezi mmoja na nusu ni chanjo ya Polio na Surua-Rubella hali iliyosababishwa na mlipuko wa Covid-19 Duniani, huku akisisitiza Serikali imekua ikinunua chanjo hizo kutoka nchi za Ulaya na Asia.

Aliongeza "Serikali inaendelea

kutoa fedha za chanjo na hadi sasa tayari imetoo zaidi ya Shilingi Bilioni 18 kwa ajili ya ununuzi wa chanjo na hivyo kuifanya Tanzania kuendelea kuwa katika kiwango cha juu cha utoaji wa chanjo kwa zaidi ya asilimia 98 kwa miaka sita mfululizo.

Hata hivyo, Dkt. Subi amesema

kuwa, Tanzania haijawahi kupata mgonjwa wa kupooza tangu mwaka 1996, jambo linalotokana na uwepo wa halilnzuri ya upatikanaji wa chanjo, huku akidai kuwa nchi ya Tanzania tayari imepata cheti cha utambuzi kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO) mwaka 2015.



Wapewa miezi sita kuongeza kasi katika kupunguza vifo vya mama na mtoto

NA WAMJW- MOSHI, KILIMANJARO

MGANGA Mkoo wa Serikali Prof. Abel Makubi ameagiza ndani ya

miezi sita (kuanzia Agosti, mwaka huu hadi Februari, mwakani), Wakurugenzi wa Hospitali, Waganga Wakuu wa mikoa,

Waganga Wakuu wa Wilaya na Waganga wafawidhi wote nchini kuongeza kasi ya kuendelea kupunguza zaidi vifo vya mama na mtoto kwa kuboresha huduma na usimamizi katika maeneo yao.

Mganga Mkoo wa Serikali alitoa agizo hilo wakati akiongea na Watumishi wa hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mawenzi - Kilimanjaro kwene ziara yake ya kukagua hali ya utoaji huduma na ujenzi wa miundombinu ya afya katika Mkoa huo Kilimanjaro.

"Wakurugenzi wakuu wa Hospitali Taifa, Kanda, Waganga Wakuu wote wa Mikoa, Wilaya pamoja na Waganga Wafawidhi wa Hospitali zote mlifanyie kazi hili suala la kuendelea kupunguza zaidi vifo vya akina mama wajawazito, nawapa miezi mitatu hadi sita, nione hali ya vifo vinaendelea kushuka zaidi kila Kanda, Mkoa, Wilaya, na Vituo vya afya. Baada ya miezi sita Serikali chini ya Wizara za AFYA na TAMISEMI tutafanya tathimini ya utendaji wenu kuhusu hili swala

na viashiria vingine vya matokeo ya uwajibikaji wenu.

Prof. Makubi aliwataka kuunda vikosi kazi ambavyo vitaongeza kasi ya kuendelea kupunguza vifo vya watoto wachanga na mama katika Hospitali na vituo vya afya, huku akiweka wazi kuwa Serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika sekta ya Afya, huku akisisitiza kuwa, uwekezaji huo hauendani kabisa na hali ya vifo vya akina mama na watoto uliopo kwa sasa.

Aidha, Prof. Makubi alisema vifo vya akina mama wajawazito na mtoto vinaweza kupungua mno nchini kama kutakuwa na uwajibikaji na kujitoa kwa kila mta kwa nafasi yake, ikiwemo uratibu mzuri baina ya watoa huduma za afya ili kuondoa ucheleweshaji wa kupata huduma kwa mama wajawazito, huku akisisitiza kuzitumia Hospitali ya taifa na za Kanda ili kubadilishana ujuzi na hospitali za ngazi ya chini na utambuzi wa viashiria vibaya kwa mjamzito wakati wa mahudhurio ya kliniki.



Wakuu wa vyuo vikuu vya afya nchini wakutana kujadili uzalishaji wa rasilimali watu sekta ya afya

NA MWANDISHI WETU, MOROGORO

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imewataka Wakuu wa Vyuo Vikuu vya Afya kuwa na mitaala ya masomo ambayo itaendana na mahitaji nchi ili kuongeza uzalishaji wa rasilimali watu wa sekta ya afya.

Katibu Mkuu Profesa Mabula Mchembe, alisema hayo mjini Morogoro wakati akifungua kikao kazi cha Wizara hiyo na Vyuo Vikuu vya Afya kuhusu uzalishaji wa Rasilimali watu wa sekta ya Afya.

Alisema tatizo la uzalishaji wa wataalamu wa sekta ya Afya lipo ndani ya Vyuo Vikuu hiyo ,hivyo kwa umoja wao wakishirikiana na mabaraza ya kitaaluma wanao wajibu wa kuandaa mitaala yenye kukidhi mahitaji na itakayochangia kuongezeka kwa waunguzi, madaktari na wafamasia wenyewe kuwa na ujuzi .

"Vyuo Vikuu vya Afya vinahitajika kuangalia na kuandaa mitaala kulingana na mahitaji ya nchi katika

kufundisha ili kupata uzalishaji wa rasilimali watu ya kutosha kwa mahitaji yaliyopo hapa nchini" alisema Profesa Mchembe.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo pia, alivishauri Vyuo Vikuu hivyo vielekeze nguvu zaidi katika kufundisha wa ujuzi ili wahitimu waweze kukidhi mahitaji ya nchi kulingana na mazingira yaliyopo.

Pia alivishauri Vyuo Vikuu hivyo kuangalia namna ya kuingiza somo la ualimu kwani kwa sasa linahitajika zaidi pamoa na Menejimenti ya utawala ili yaende sambamba na ufundishaji wa masomo ya Medicine (uuguzi, ufamasia na udaktari).

"Mimi kitu ambacho nimekuja kulingundua pia kuna somo moja tunaliacha ambalo tunatakiwa tuiigize kwenye Wizara ya Elimu , Sayansi na Teknolojia ni la ualimu ambalo ni mojawapo unapofundishwa kwenye 'medicine' lazima ufundishe 'basic Knowledge' yaualimu kwa maana mwisho wa siku wewe (Daktari, Muuguzi na mfamasia) ni mwalimu "

alisema Profesa Mchembe.

Kuhusu somo la Menejimenti ya Utawala ambalo linapaswa kuingizwa ingawa zamani lilikuwepo kwenye medicine , alisema kwasasa ni la muhimu kwa vile baadhi ya Waganga wakuu wa wilaya ni vijana na wanahitajika kupata ujuzi kwenye suala la uongozi na utawala ili wawe ni viongozi wazuri.

Katibu mkuu pia, alitumia fursa hiyo kuvikumbusha Vyuo vikuu vya afya, kabla ya kuanzishwa kwa kozi mpya vishirikiane kwanza na wataalamu wengine wakiwemo wa wizara hiyo ili endapo kozi hiyo zina mahitaji nchini na sikuinga mitaala ya kozi kutoka nje ya nchi ambapo baadaye wahitimu wake wanashindwa kuingia kwenye mfumo wa utumishi wa umma.

Naye Mkurugenzi wa Mafunzo wa Wizara hiyo , Dk Saitore Laizer, kabla ya kumkaribisha Katibu Mkuu kufungua kikao kazi hicho, alisema kikao hicho kilichohudhuriwa na Makamu wakuu wa vyuo, wasaidizi wa makamu wakuu wa vyuo na taasisi za kisekta za kielimu.

Dk Laizer, alisema lengo lilikuwa ni kujadiliana kwa sauti moja ya watunga sera na watekelezaaji wa sera kuangalia changamoto ya uhaba kwa baadhi ya wataalamu wa afya, kutafuta ufumbuzi na utatuzi wake utakaolenga kuongeza uzalishaji wa rasilimali watu wasekta ya afya.

Kwa upande wake Mkuuu Chuo KikuuKishiriki cha Tiba cha Kikristo Kilimanjaro (KCMUCo) , Profesa Ephata Kaaya , akizungumza kwa niiba ya washiriki wenzake alisema viongozi wa vyuo watatekeleza changamoto hizo ili kuweza kutoa wataalamu wa afya wanaohitajika na wenyewe sifa za kufanyakazi kulingana na mazingira ya hapa nchini.

"Ni jambo la busarakwakuitishwakwakikaohiki nakimekuwa na mwanzo mzuri kwa kukutana na kujadiliana kwa pamoa iliyuo vikuu vyetu viweze kutoa na kutengeneza rasilimali watu ambao wataendana na mahitaji ya Taifa " alisema Profesa Kaaya.

Wagonjwa wa Sikoseli wapewa ahueni ya matibabu

NA WAJMW-DODOMA

Wagonjwa wa Sikoseli nchini wamepewa unaafuu wa gharama na upatikanaji wa dawa baada ya Serikali kuptita Wizara ya Afya kuweka mikakati Madhubuti inayolenga kuboresha huduma kwa wagojwa hao.

Hayo yamesemwa mbele ya Waandishi wa Habari jijini Dodoma na Kaimu Mkurugenzi wa huduma za Tiba wa Wizara Afya Dkt. James Kiologwe aliywakilisha Mganga Mkuu wa Serikali katika kilele cha maadhisho ya mwezi wa Sikoseli duniani.

Dkt. Kiologwe alisema mionganoni mwa hatua zilizochukuliwa na Serikali ni Pamoja na kujumuisha Sikoseli katika Mpango Mkakati wa Taifa wa pili wa magonjwa yasiyoambukiza wa mwaka 2016-2020 na kuhakikisha kliniki za wagonjwa wa Sikoseli zinaanzishwa katika mikoa yote nchini ikiwa ni pamoja na upatikanaji rahisi wa dawa ya 'Hydroxyurea' ambayo itaingizwa katika muongozo wa matibabu vilevile kuwekwa katika orodha ya dawa zinazolipiwa na Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF).

ya Afya (NHIF).

Aidha, Dkt. Kiologwe alisema Serikali itahakikisha kwamba vipimo vya papo kwa papo (Sickle Scanner) na dawa ya HU vinaingia kwenye Kinadi cha bei cha Bohari ya Dawa (MSD Price Catalogue).

Pamoja na hayo Dkt. Kiologwe alisema Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kuielimisha jamii ili kuwa na uelewa wa pamoja juu ya ugonjwa huu ambapo inatarajia kwa kiasi kikubwa itapunguza na hatimaye kuondoa unyanyapaa kwa wagonjwa wenyewe Sikoseli.

Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya duniani (WHO) inaonesha kila siku Zaidi ya Watoto 1,000 huzaliwa na Sikoseli huku Tanzania takwimu zinaonesha Zaidi ya Watoto 11,000 huzaliwa na ugonjwa wa Sikoseli kila mwaka, sawa na kusema Watoto 8 kati ya 1,000 huzaliwa na ugonjwa huu.

Maadhisho ya mwezi wa Sikoseli hufanya mwezi Septemba kila mwaka duniani kote na mwaka huu yalikua na kaulimbiu iliyosema "Ijue Sikoseli, epuka unyanyapaa".

Na WAJMW-Dodoma

Wagonjwa wa Sikoseli nchini wamepewa unaafuu wa gharama na upatikanaji wa dawa baada ya Serikali kuptita Wizara ya Afya kuweka mikakati Madhubuti inayolenga kuboresha huduma kwa wagojwa hao.

Hayo yamesemwa mbele ya Waandishi wa Habari jijini Dodoma na Kaimu Mkurugenzi wa huduma za Tiba wa Wizara Afya Dkt. James Kiologwe aliywakilisha Mganga Mkuu wa Serikali katika kilele cha maadhisho ya mwezi wa Sikoseli duniani.

Dkt. Kiologwe alisema mionganoni mwa hatua zilizochukuliwa na Serikali ni Pamoja na kujumuisha Sikoseli katika Mpango Mkakati wa Taifa wa pili wa magonjwa yasiyoambukiza wa mwaka 2016-2020 na kuhakikisha zinaanzishwa katika mikoa yote nchini ikiwa ni pamoja na upatikanaji rahisi wa dawa ya 'Hydroxyurea' ambayo itaingizwa katika muongozo wa matibabu vilevile kuwekwa katika orodha ya dawa zinazolipiwa na Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF).

Aidha, Dkt. Kiologwe alisema

Serikali itahakikisha kwamba vipimo vya papo kwa papo (Sickle Scanner) na dawa ya HU vinaingia kwenye Kinadi cha bei cha Bohari ya Dawa (MSD Price Catalogue).

Pamoja na hayo Dkt. Kiologwe alisema Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kuielimisha jamii ili kuwa na uelewa wa pamoja juu ya ugonjwa huu ambapo inatarajia kwa kiasi kikubwa itapunguza na hatimaye kuondoa unyanyapaa kwa wagonjwa wenyewe Sikoseli.

Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya duniani (WHO) inaonesha kila siku Zaidi ya Watoto 1,000 huzaliwa na Sikoseli huku Tanzania takwimu zinaonesha Zaidi ya Watoto 11,000 huzaliwa na ugonjwa wa Sikoseli kila mwaka, sawa na kusema Watoto 8 kati ya 1,000 huzaliwa na ugonjwa huu.

Maadhisho ya mwezi wa Sikoseli hufanya mwezi Septemba kila mwaka duniani kote na mwaka huu yalikua na kaulimbiu iliyosema "Ijue Sikoseli, epuka unyanyapaa".

HABARI KATIKA PICHA

ZIARA YA MKURUGENZI WA HUDUMA ZA UUGUZI NA UKUNGA MKOANI SINGIDA, MANYARA, ARUSHA, KILIMANJARO NA TANGA



Wauguzi na Wakunga wasiohuisha leseni zao kuchukuliwa hatua

NA. CATHERINE SUNGURA - DODOMA.

Wauguzi na Wakunga ambao watakuwa hawajahuisha leseni zao ndani ya miezi sita watachukuliwa hatua, ikiwemo kufutwa kwenye daftari la Uuguzi na Ukunga, hivyo kutoruhusiwa kutoa huduma kwenye vituo vya afya vya umma au binafsi nchini.

Yalielezwa hayo na Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga, Bi. Agnes Mtawa, kwenye kikao kazi cha kuwajengea uwezo wa kusimamia maadili na utendaji kazi Wauguzi Wakuu wa Wilaya kilichofanyika hivi karibuni huko Jijini Dodoma.

"Nito rai kwa Wauguzi na Wakunga ambao hawajahuisha leseni zao ndani ya miezi sita, sheria inamtaka msajili awafute katika daftari la Uuguzi na Ukunga na kama watafutwa hawatakuwa na sifa ya uuguzi na ukunga nchini," alisema Bi. Mtawa.

Aidha, Msajili huyo alisema hadi sasa

ni asilimia 75 ya wauguzi na wakunga waliohuisha leseni zao na asilimia 25 walibaki bado hawajahuisha.

"Hivyo bado tunaendelea kuangalia kanzidata yetu huenda katika hii asilimia 25 wapo ambao pengine wamefariki, wamestaafu au wamebadilisha kada.

"Lakini kwa wale ambao bado wanatoa huduma za uuguzi na ukunga tunawakumbusha kuwa na leseni kwa mujibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga Namba moja ya Mwaka 2010 na wale watakaoshindwa kuhuisha leseni zao sheria inasilitiza kwamba hawaruhusiwi kuendelea kutoa huduma ya Uuguzi na Ukunga.

Aliongeza "Taarifa imeshapelekwa kwa wahusika na orodha imetayarishwa kwa wale waliohuisha leseni zao, mchakato utakapokamilika wale ambao hawatahuisha watakuwa wamejifuta wenyewe na hawatakuwa na sifa ya kuendelea kutoa huduma za afya na waajiri wao watatakiwa kuwachukulia



hatua za kuwafuta kazi kwenye vituo vya Umma na vile vya binafsi.

Sambamba na hilo, Bi. Agnes Mtawa, aliwakumbusha Wauguzi kuzingatia maadili kwa kufuata taratibu, kanuni na Sheria kwa sababu kumekuwa na malalamiko ya hapa na pale kuhusu utoaji wa huduma kwenye vituo vya afya.

"Hivyo kuwakutanisha Wauguzi wakuu wa Wilaya kama viongozi na wasimamizi ni chachu katika kukumbushana taratibu na jinsi ya kusimamia miongozo na kanuni.

Naye Mwakilishi kutoka Ofisi ya Rais Tamisemi Kalidushi Charles alisema malalamiko mengi yanaelekezwa kwa wauguzi kwani sehemu kubwa ndiyo wanaopokea na kukaa (kuwashudumia) wagonjwa kwa muda mrefu, hivyo wanapaswa kusimamia sheria, huku

akisisitiza wasioneane haya bali wawajibishane ili huduma za afya ziwe nzuri.

"Tunafahamu sasa hivi Serikali ya Awamu ya Tano imeboresha miundombinu kumekuwa na vituo vingi vya kutolea huduma za afya ambavyo vinafanya upasuaji kwa hiyo vituo hivi havitokuwa na maana kama sisi wasimamizi wa hizo huduma hatutosimamia vizuri ili wananchi waweze kupata huduma kama adhima ya Serikali," alisema.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Wakuu wa Wauguzi ambaye pia ni Muuguzi Kiongozi kutoka Wilaya ya Bukombe, Fadhili Meshack, alisema mafunzo hayo yanawajengea uwezo viongozi kwa ajili ya kupanua wigo wa uelewa ili kuweza kuwasimamia na kuwasaidia wauguzi wanaowaongoza.

Wamiliki wa Maabara Binafsi za Afya wahimizwa kufuata sheria

NA. WAMJW - DAR ES SALAAM

Wamiliki wa Maabara Binafsi za Afya wameelekezwa kufuata sheria na taratibu zinazosimamia uendeshwaji wa maabara hizo ili wagonjwa wapate majibu sahihi yatakayopelekea huduma bora za matibabu.

Hayo yamebainishwa na Msajili wa Bodii ya Maabara Binafsi za Afya nchini, Bw. Dominic Fwiling'afu, wakati wa ukaguzi wa Maabara Binafsi za Afya katika Wilaya zote za Jiji la Dar es Salaam.

Bw. Fwiling'afu alisema ukaguzi huo umefanya kwa lengo la kuangalia hali ya utoaji wa huduma za maabara Mkoani Dar es Salaam ili kuhakikisha watanzania wanapata huduma bora za maabara ambazo zitawasaidia matabibu kutoa huduma bora kwa wagonjwa. "Katika ukaguzi wetu tumepita katika Wilaya zote

za Jiji la Dar es Salaam, tumefanya ukaguzi, tumetoa elimu, ushauri na maelekezo magine ili kuboresha huduma.

"Lakini pia kuna baadhi ya maabara

tumelazimika kuzifungia kwani

zimekua zikiendeshwa kwa kukiuka

sheria Na. 10 ya Mwaka 1997 pamoja

na kuhatarisha maisha ya Watanzania

wanaofika kupata huduma katika vituo

hivyo," alisema Bw. Fwiling'afu.

Alisema pamoja na kuzifungia

baadhi ya maabara ambazo zimekua

zikiendeshwa kwa kukiuka sheria zipo

zilizopongezwa kwa kutoa huduma

bora kwa kufuata sheria na miongozo

na hivyo kupelekeea wananchi kupata

huduma bora.

Kwa upande wake Mratibu wa huduma za Maabara Wilaya ya Ilala Petrobras Hassan alishukuru Wizara ya Afya kwa kufanya ukaguzi huo

katika Jiji la Dar es Salaam kwa kuwa

kuna maabara nydingi na zinahitaji

kujengewa uwezo ili zitoe huduma bora kwa wananchi.

"Naishukuru sana Wizara ya Afya kupitia Bodii ya Maabara Binafsi za Afya, kwa kuja kufanya ukaguzi huu, mimi kama Mratibu nimefarijika sana maana ninaowasimamia wamepata elimu, ushauri pamoja na maelekezo magine yanayolenga kuboresha huduma hivyo nashauri ukaguzi huu ufanyike mara kwa mara ili kuendelea kuboresha huduma," alisema Bw. Petrobas.

Mtaalam wa maabara kutoka Kituo cha Ibrahim Haji cha Jijini Dar es Salaam, Bw. Deogratious, alishukuru Wizara ya Afya kwa kufanya ukaguzi na kutoa mafunzo kwa wataalamu wa maabara jambo ambalo limewaongeza ujuzi na maarifa katika kufanya kazi zao za kila siku na kuhakikisha wananchi wanapata majibu sahihi kwa wakati ili kupata tiba bora.





Majibu ya vipimo yakaguliwe, yasainiwe mapema kabla mgonjwa hajarudi kuyafuata

NA. RAYSON MWAISEMBA- ARUSHA

Licha ya kuendelea kufanya Juhudi kubwa katika kupunguza vifo nya mama na mtoto, bado tuna namba kubwa ya vifo hivyo, kama Serikali inaonegeza vituo na kuboresha huduma, kwanini vifo bado vipo juu, na mara nyingi vifo vingi vinaweza kuzuiliika

Agizo hilo lilitolewa na Mkurugenzi wa Tiba Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dkt. Grace Maghembe alipofanya ziara ya kukagua hali ya utoaji huduma za afya na kuzungumza na watumishi katika hospitali hiyo kuhusu uboreshwaji wa huduma za afya ambapo pia aliwataka watoa huduma za afya wote nchini kufanya kazi kwa kushirikiana baina yao na viongozi wao ili kuboresha huduma za afya nchini.

"Ninawaomba sana tufanye kazi kwa umoja na ushirikiano, migongano na misuguano haileti maana yoyote katika kuwashudumia Watanzania, kama kuna mwenzetu katoka nje ya mstari, tuambiane ukweli na tuonyane bila kuleta misuguano". Alisema Dkt. Grace.

"Serikali imeendelea kujenga vituo vya kutolea huduma za afya, na kuboresha viliyio-chakaa, hivyo ni wakati wa watoa huduma kushirikiana kwa karibu na kufanya kazi kwa juhudi na ubunifu ili kuleta matokeo chanya katika utoaji huduma," alisisitiza.

Hata hivyo, Dkt. Grace alisisitiza agizo la Mganga Mkuu wa Serikali juu ya kuongeza jitihada katika mapambano ya kuendelea kupunguza vifo nya mama na mtoto katika vituo vya kutolea huduma za afya, ndani ya miezi sita.

"Licha ya kuendelea kufanya Juhudi kubwa katika kupunguza vifo nya mama na mtoto, bado tuna namba kubwa ya vifo hivyo, kama Serikali inaonegeza vituo na kuboresha huduma, kwanini vifo bado vipo juu, na mara nyingi vifo vingi vinaweza kuzuiliika". Alisema Dkt. Grace.

Mbali na hayo, Dkt. Grace alitoa rai kwa viongozi wa hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha - Mount Meru kuhakikisha wanajiongeza ili kuongeza ukusanyaji mapato, jambo litalosaidia katika kuboresha huduma kwa wagonjwa.

Pia, Dkt. Grace aliagiza kila muuguzi ni lazima awe na mpango wa huduma ya mgonjwa wake (nursing care plan), ikiwa ni sehemu ya kuboresha huduma kwa

mgonjwa anaye mhudumia.

Naye Mkurugenzi wa uhakika ubora wa huduma Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dkt. Eliakim Eliud alitoa rai kwa viongozi kushughulikia malalamiko ya wagonjwa kwa haraka, huku akiagiza namba za viongozi zibandikwe maeneo yanayoonekana na ziandikwe kwa kuonekana.

Aidha, aliwataka watoa huduma kutoa majibu kwa wagonjwa haraka pindi wanapowahudumia ili kufahamu wanansumbuliwa na shida gani, kuliko kuwapa dawa bila kuwapa mrejesho wa magonjwa yanayomsumbia.

Dkt. Eliakim aliwataka pia watumishi wote katika maeneo ya kutolea huduma za afya kuboresha maadili, ikiwemo matumizi mazuri ya lugha kwa wanaokuja kupata huduma, kuanzia wanapoingia getimi mpaka wanapomaliza kupata huduma, ili kupunguza malalamiko yasiyo na ulazima.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Mkoa wa Arusha Dkt. Alfello Sichalwe aliishukuru Serikali kuititia Wizara ya Afya kwa kuendelea kuboresha huduma katika Mkoa wa Arusha, huku akiahidi kuendelea kusimamia vizuri hali ya afya ikiwemo kupunguza vifo nya mama na mtoto katika Mkoa huo.

“

Wizara ya Afya Tanzania

Tushirikiane kupambana dhidi ya magonjwa yasiyo ambukiza – Prof. Makubi

NA.RAYSON MWAISEMBA- KILIMANJARO

MGANGA Mkuu wa Serikali Prof. Abel Makubi ametoa wito kwa watoa huduma za Afya kushirikiana kwa pamoja kwa kutoa elimu, katika mapambano dhidi ya magonjwa yasiyo ambukiza yanayosababishwa na mtindo wa maisha ikiwemo ulaji usiofaa, matumizi ya vileo na kutofanya mazoezi.

Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Makubi alitoa rai hiyo alipotembelea Hospitali ya Rufaa ya kanda ya Kaskazini (KCMC) kukagua hali ya utoaji huduma za Afya katika Hospitali hiyo kwa wananchi.

Prof. Makubi alisema ni muhimu watoa huduma za afya kuungana kwa pamoja kushirikiana kwa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu magonjwa yasiyo ambukiza (NCD), kwa njia ya kuwafuata wagonjwa katika maeneo yao, jambo ambalo litasaidia kupunguza mzigo wa wagonjwa katika hospitali za Rufaa nchini.

"Mshirikiane kwa pamoja kutoa Elimu ya ufahamu, na kupima angalau mara 2 kwa mwaka juu ya magonjwa yasiyo ambukiza kuitia njia ya kuwafuata wateja katika maeneo yao na kuwafanyia upimaji (outreach program)" alisema Prof. Makubi.

Hata hivyo, Prof. Makubi alitoa rai kwa watoa huduma za afya kuhakikisha wanatoa huduma kwa wakati kwa wagonjwa ili kuepusha msongamano unaoweza sababisha mlipuko wa magonjwa mengine katika hospitali na kupunguza usumbufu kwa wagonjwa.

Aidha, Prof. Makubi ameridhishwa kwa kiasi kikubwa hali ya utoaji huduma katika Hospitali hiyo, huku akiwataka kuongeza jitihada ili kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi na kupunguza malalamiko yanayoweza kuepukika kwa urahisi.

"Mimi kwa KCMC, sipati malalamiko mengi sana, simamieni katika ubora huo, na mhakikishe mnaongeza Juhudi zaidi, na kwa hilo nawapong'enza sana sana" alisema Prof. Abel Makubi.

Prof. Makubi aliwapongeza watumishi wa Hospitali ya KCMC wakiongozwa na Mkurugenzi wao Prof. Gileard Masenga kwa kuanzisha mradi wa uzalishaji wa gesi ya oksijeni, jambo linalosaidia kuongeza mapato na kuokoa kiasi kikubwa cha pesa ambacho kingetumika kununua mitungi ya gesi, na pesa hizo kuelekezwa katika kuboresha huduma kwa wananchi.

Naye, Mkurugenzi wa huduma za tiba Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dkt. Grace Maghembe aliwataka watumishi kutobweteka, katika kuwashudumia wananchi, licha ya kazi nzuri ambayo inaendelea kufanywa na uongozi kwa kushirikiana na Mkoa.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa uhakika ubora huduma Wizara ya Afya Dkt. Eliakim Eliud aliwataka watoa huduma kuhakikisha wanafuata miongozo ya kujikinga ya utoaji huduma (IPC guidelines) wakati wa kuhudumia wagonjwa ili kujikinga wao na wagonjwa wanaowahudumia.



“
*Mimi kwa
KCMC, sipati
malalamiko
mengi sana,
simamieni katika
ubora huo, na
mhakikishe
mnaongeza
Juhudi zaidi,
na kwa hilo
nawapong'enza
sana sana*

Viwango utoaji huduma Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma viboreshwe – Serikali



“

Kama Wizara tumejipanga vizuri kwa kuhakikisha chanjo zote zinakuwepo kwa wakati kwenye vituo ya kutolea huduma za afya na kuhakikisha watoto wote waliokuwa wanatarajia kupata chanjo wanapata na watoa huduma wanachukua tahadhari zote za kujikinga na ugonjwa huu

NA. CATHERINE SUNGURA, WAMJW - DODOMA

UONGOZI wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma umeagizwa kuboresha huduma za tiba kwa wananchi wanaofika kupata huduma za afya hospitalini hapo.

Maagizo hayo yalitolewa na Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi kwa uongozi huo alipofanya ziara ya kushtukiza katika hospitali hiyo na kushuhudia changamoto mbalimbali ikiwemo baadhi ya wagonjwa kuchelewa kupewa huduma, Madaktari bingwa kutowaona wagonjwa kwa wakati na huduma za vipimo kuchelewa.

"Yapo mazuri tumeona mnayofanya kwa wananchi na tunawapongeza, ila lazima kuangalia upande wa pili ambayo wananchi wanayataka, kwa yale mapungufu tuliyoyaona tungependa kuona yanaboreshwu haraka ili hospitali hii iwe ya mfano kwa hospitali zote za rufaa za mikoa kwa kutoa huduma zilizo bora," alisema.

Prof. Makubi alisema hospitali hiyo inatakiwa kuonesha mfano kuanzia utoaji wa huduma bora kwa mteja pamoja, kupunguza muda wa wagonjwa kusubiri huduma, upatikanaji wa wauguzi na mabingwa wanapohitajika na usafi wa wodi kwani ndio chachu ya wananchi

wengi kufika hapo na kupata huduma kabla hawajapewa rufaa ya kwenda Hospitali kubwa kama Benjamin Mkapa.

Aidha, Mganga Mkuu huyo aliutaka uongozi na watumishi wa hospitali hiyo kutambua majukumu yao kwa kuonesha kuwajali wananchi wote na kuwataka kuweka utaratibu usio na usumbufu kwa wagonjwa na kupatiwa huduma kwa wakati.

Prof. Makubi alionesha kusikitishwa alipokuta wodini baadhi ya wagonjwa wamelazwa na hawajaonwa na wataalamu mabingwa kwa zaidi ya siku tatu, wauguzi wakiwa hawajaambatana na madaktari katika kuzungukia wagonjwa.

Aidha, alikuta madaktari wa vitendo (interns) wakifanya "procedures" peke yao bila uangalizi na baadhi ya wagonjwa wengine wakiwa wamelazwa chini wakati vitanda viko wazi pamoja na mazingira ya wodi hayakuwa ya kuridhisha na kukosekana kwa mpangilio wa vifaa (5S)

"Lazima watumishi mijitambue mko wapi kwani awamu hii ni ya kuwajali wanyonge na kufanya kazi kwa bidii ndio kanuni ya awamu hii hapa kazi tu," alisisitiza Prof. Makubi.

Prof. Makubi alielekeza madaktari wa hospitali hiyo kufanya kazi

kwa ushirikiano na wauguzi katika kuwashudumia wagonjwa katika wodi, kuleta mabadiliko kwa kutengeneza miongozo mbalimbali ya kusimamia huduma na kuacha kufanya kazi kwa mazoea ili kila mwananchi anayefika ahudumiwe kwa wakati, huduma inayostahili.

Kwa upande mwagine, Mganga Mkuu huyo wa Serikali, aliiptaka hospitali hiyo kuboresha idara ya huduma kwa wateja (Customer Care) kwani hakuna mgonjwa anayependa kuchelewa kupata huduma hivyo lazima kutoa huduma bora na zinazohitajika kwa wananchi wote.

Prof. Makubi alielekeza uongozi wa hospitali hiyo kuhakikisha mashine za maabaraha ambazo zimeishiwa vitendanishi zinaanza kufanya kazi haraka.

"Ni vizuri mkapunguza muda wa kusubiri majibu ya vipimo vyatya damu, X-ray, ultrasound, moyo na vipimo vingine," alielekeza Prof. Abel Makubi.

Prof. Makubi aliagiza hospitali zote nchini zifanyie kazi changamoto alizoziona hapo Dodoma, aliagiza pia idara ya ukaguzi wa huduma bora kutoka wizarani wafanye ufuutiliaji wa utoaji wa huduma mikoani, wilayani na vituo vyatya kila mwezi na kutoa taarifa kwake.

Simamieni usajili wa dawa za asili, wapeni elimu ya kutosha watengenezaji - Prof. Mchembe

NA.RAYSON MWAISEMBA-DODOMA

KATIBU MKUU Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto - Idara Kuu ya Afya, Prof. Mabula Mchembe, amewaaigiza Baraza la Tiba Asili na Tiba mbadala na Mamlaka zote katika Mikoa na Halmashauri nchini kusimamia usajili wa dawa za asili kwa kutoa elimu ya kutosha kwa waganga na watengeneza dawa wa tiba asili.

Prof. Mchembe alitoa agizo hilo wakati wa kufunga maadhimisho ya Siku ya Tiba Asili ya Mwafrika yaliyofanyika hivi karibuni katika viwanja vya Mwl. Nyerere Jijini Dodoma, yenye kauli mbiu ya "Miongo miwili ya Tiba Asili Afrika 2001 mpaka 2020 Nchi zina mafanikio gani".

"Kwa maana hiyo basi nawaagiza Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala na Mamlaka zote katika Mikoa na Halmashauri nchini kusimamia usajili wa dawa za asili kwa kutoa elimu ya kutosha kwa waganga na watengeneza dawa wa tiba asili," alisema Prof. Mchembe.

Aliendelea kusisitiza kuwa, ni vyema Baraza la tiba asili na Mamlaka zote nchini, kushirikiana na taasisi zote zinazohusiana na tiba asili hususan Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kutohana na kuwepo kwa kitengo kinachohusiana na mimea.

Prof. Mchembe alisema katika kuadhimisha miaka 18 ya Siku ya Tiba Asili ya Mwafrika, Serikali kupitia Wizara



ya Afya imefanya mambo mengi ikiwemo, kuitambua huduma ya tiba asili katika Sera ya Afya.

"Kuanzia kutungwa kwa Sheria ya Tiba Asili na Tiba Mbadala Namba 23 ya mwaka, kutengenezwa kwa kanuni na miongozo mbalimbali ya Tiba Asili na Tiba Mbadala mwaka, kuanza kutoa mafunzo kwa Waratibu na watoa huduma wa tiba asili nchini.

Alibainisha hadi sasa Baraza hilo limeshasajili dawa 30 huku akiweka wazi kwamba kiasi hicho cha dawa zilizosajiliwa ni kidogo ukilinganisha na uhalisia.

Aidha Prof. Mchembe, aliliagiza Baraza hilo na Mamlaka zote katika Mikoa

na Halmashauri nchini kuhakikisha zinasimamia usajili wa dawa za asili kwa kutoa elimu ya kutosha kwa waganga na watengeneza dawa wa tiba asili.

Mbali na hayo Prof. Mchembe alitoa wito kwa Wataalamu wa tiba asili na tiba mbadala nchini kutumia fursa kwa kuanzisha viwanda vidogo na vyta kati vyta kuchakata dawa za asili kwa lengo la kuongeza ubora na hivyo thamani yake.

"Nitoe wito kwa Waganga na wadau wa Tiba Asili kutumia fursa iliyopo ya Tanzania ya Viwanda kwa kuanzisha viwanda vidogo na vyta kati vyta kuchakata dawa za asili kwa lengo la kuongeza ubora na hivyo thamani yake," alitoa rai.

“

Nitoe wito kwa Waganga na wadau wa Tiba Asili kutumia fursa iliyopo ya Tanzania ya Viwanda kwa kuanzisha viwanda vidogo na vyta kati vyta kuchakata dawa za asili kwa lengo la kuongeza ubora na hivyo thamani yake...





Wafamasia zingatieni maadili ya taaluma yenu kuboresha utoaji huduma

“

Serikali nia njema katika kuboresha huduma za afya nchini, utakuta hospitali fulani ina vifaa vizuri sana vya kufanya kazi lakini haina wataalam wa kuvitumia

N.A.EMMANUEL MALEGI-MOROGORO

Wafamasia nchini ni lazima wazingatie maadili na kutumia taaluma walijonayo ipasavyo ili kutoa huduma bora kwa wananchi, ameagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Mabula Mchembe.

Agizo hilo alilitoa wakati alipokuwa akifunga semina inayojumuisha wadau wa Mnyororo wa Ugavi na Usambazaji wa Bidhaa za Afya kutoka Sekta mbalimbali za Serikali na Binafsi waliokutana Mkoani Morogoro.

“Ninawataka Wafamasia wote mbadilike kulingana na mazingira yaliyopo, hivi sasa nchi imeingia kwenye uchumi wa kati, hii ina maana mboreshe utaalamu wenu ili kukidhi mahitaji ya nchi.

“Corona imekuja na faida kubwa, imetufanya sasa tunaweza kutengeneza vitakasa mikono vyetu (Hand Sanitizer) na barakoa jambo ambalo hapo awali halikuwepo,” alisema Prof. Mchembe.

Prof. Mchembe alisisitiza kuboresha kwa huduma za dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya zikiwemo Zahanati na vituo vya afya vya umma kuhakikisha dawa zote muhimu zinapatikana ili mwananchi anapofika kupata huduma asizikose na kulazimika kwenda kununua kwenye maduka ya watu binafsi.

Aidha, Prof. Mchembe aliwataka wataalamu hao kutochagua vituo vya kazi kwani kwa kufanya hivyo wanaweza kuwa wanadidimiza taaluma yao kwa kufanya kazi maeneo ambayo hayana vifaa.

“Serikali nia njema katika kuboresha huduma za afya nchini, utakuta hospitali fulani ina vifaa vizuri sana vya kufanya kazi lakini haina wataalam wa kuvitumia,” alisema Katibu Mkuu huyo.

Katika kututua changamoto hizo, Prof. Mchembe alimuagiza Mfamasia Mkuu wa Serikali, Daudi Msasi kuweka mwongozo mzuri katika kuwapangia vituo vya kazi Wafamasia na wataalam wengine ili wananchi waweze kupata huduma bora za afya popote walipo.

Prof. Mchembe alisisitiza matumizi ya data katika kutoa huduma na kutunza kumbukumbu kuititia mifumo ya GOTHOMIS na mingineyo ili kurahisisha utoaji wa huduma na kutunza rekodi za wagonjwa, pia kuweka mnyororo wa huduma zote za hospitali katika hali nzuri.

Wakunga wajidhatiti kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi nchini

NA EMMANUEL MALEGI-DODOMA

Wadau wa Uuguzi na Ukunga wamekutana na kupanga mikakati ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wachanga kwa kuhakikisha huduma zinakuwa bora ikiwa ni Pamoja na kushirikisha walimu wa vyuo mbalimbali vinavyozalisha wanafunzi wa taaluma hiyo.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi wa huduma na Ukunga na Uuguzi kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Bi. Ziada Sellah wakati akifungua mafunzo wezeshi yakujadili namna ya uboreshaji wa huduma za Ukunga nchini kwa niaba ya Mganga mkuu wa Serikali ambapo mafunzo hayo yaliwashirikisha Wizara ya afya, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, wakufunzi wa vyuo na Chama cha Wakunga Tanzania (TAMA) kwenye hospitali ya Benjamin Mkapa jijini hapa.

"Tumeangalia kwa upana wake na kuweka mikakati mbalimbali ya jinsi huduma zinazotolewa na wakunga kwa wajawazito ikiwa ni Pamoja na kuwapa mazingira wezeshi, huduma nzuri kwa wateja lakini pia tumewashirikisha walimu wa vyuo vyaa ukunga ili wafundishe somo la huduma kwa mteja ili isijekua ni kitu kipyaa kwa wanafunzi wanapoingia

kazini". Alisema Bi. Ziada.

Bi. Ziada alisema Wizara kuptitia kurugenzi ya Uuguzi na ukunga itahakikisha wakunga wanapata mafunzo wakiwa maeneo yao ya kazi kuptitia kwa wauguzi wakuu wa Wilaya na Mikoa pamoja na wauguzi viongozi ili kuweza kuboresha ukunga lengo likiwa ni kupunguza vifo vitokavyo na uzazi.

"Tumeangalia kwa upana kuanzia huduma zinapoanza kutolewa upande wa huduma ya Uzazi, Mama na Mtoto pale mama anapoanza kliniki na kuelekeza jinsi gani ya kutoa huduma ikiwemo vidokezo hatarishi kwa mama mjamzito pamoja na kutoa rufaa nmapema endapo kesi hawatoiweza, hivyo tutawajengea uwezo wakunga kwani asilimia 90 ya akina mama wote wanaojifungua wanahudumiwa na wakunga".

Alisitisiza Bi. Ziada.

Naye Rais wa Chama cha Wakunga Tanzania Chama cha Wakunga nchini (TAMA) Bi. Fedy Mwanga alisema chama kimejidhatiti kutoa elimu kwa wauguzi na wakunga nchini kuhusiana na huduma bora za uzazi kwa mama mjamzito kabla na baada ya kujifungua lengo likiwa ni kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

Alisema chama hicho kinaandaa makongamano kwa ajili ya wakunga

nchini ili waweze kupata elimu na kukumbushwa maadili katika utoaji wa huduma pale mama mjamzito anapofika katika sehemu ya kutolea huduma za afya.

"Tumeita wadau mbalimbali kwa ajili ya kuendeleza shughuli zetu za utetezi wa kuimarisha shughuli za ukunga Tanzania kwa kujua kabisa vifo vitokanavyo na uzazi nchini bado viko juu na vinazuilika, kwa kutambua umuhimu wa huduma za ukunga katika kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi tunakutana ili kukumbushana wajibu wetu katika kupunguza vifo hivyo". Amesema Bi. Fedy.

Bi. Fedy alisema mkunga akiwa na stadi zinazostahili na akisimamizi vizuri na kufanya kazi katika mazingira wezeshi anawenza kumuhudumia mama na kupunguza vifo kwa asilimia 87 hivyo chama cha wakunga nchini kina wajibu wa kufanya vikao na wadau ili kuweza kujadili namna wanavyowenza kufanikisha mazingira wezeshi kwa wakunga nchini.

Wakati huo huo Msimamizi wa huduma za Uuguzi na Ukunga kutoka OR-TAMISEMI Dinya Atinda alisema wataendelea kuboresha na kusimamia huduma za uuguzi na ukunga kwenye hal mashauri zote nchini ili watoa huduma ngazi zote wanapata mafunzo na usimamizi mzuri ili kuendelea



“Tumeangalia kwa upana kuanzia huduma zinapoanza kutolewa upande wa huduma ya Uzazi, Mama na Mtoto pale mama anapoanza kliniki na kuelekeza jinsi gani ya kutoa huduma ikiwemo vidokezo hatarishi kwa mama mjamzito pamoja na kutoa rufaa nmapema endapo kesi hawatoiweza, hivyo tutawajengea uwezo wakunga kwani asilimia 90 ya akina mama wote wanaojifungua wanahudumiwa na wakunga”

MIUNDOMBINU YASAIKIA HUDUMA YA DAMU SALAMA KANDA YA MAGHARIBI

NA. CATHERINE SUNGURA-TABORA

“

Kama kanda hatujachoka kuhamasisha wananchi licha ya changamoto ya uelewa kwa jamii kuhusu uchangiaji damu,hivyo tumejipanga kuendelea kutoa elimu kwenye makundi yote ili tuweze kuwa na damu za kutosha kwenye hospitali zetu

Imeelezwa kuwa kuboreshwa kwa miundombinu imesaidia kwa kiasi kikubwa huduma ya damu salama kwenye Kanda ya Magharibi ambayo inahudumia mikoa ya Tabora,Katavi,Singida na Kigoma.

Kaimu Meneja wa kanda hiyo Bi. Zaitun Abdalah aliyasema hayo wakati wa kampeni ya kukusanya damu kwenye shule ya sekondari Mabama iliyoko Manispaa ya Tabora.

"Kwa kiasi kikubwa uboreshwaji wa barabara umesaidia sana kurahisisha upatikanaji wa mahitaji wa damu salama kwenye mikoa hii tunayohudumia ambayo inayo eneo kubwa kijirografia hivyo inapohitajika damu kwenye vituo yetu vya kutolea huduma tunawapatia kwa wakati"Alisema.

Kwa upande wa wiki hii ya kampeni ya kukusanya damu ilioanza tarehe 21 mwezi huu na kumalizika tarehe 25 ,Kaimu Meneja huyo alisema Kanda yake imeweka lengo la kukusanya chupa 100 kwa siku na

chupa 500 zinazotarajiwa kukusanya kwa wiki.

Aliongeza kuwa kwa mkoa wa tabora timu yake imejipanga katika ukusanyaji wa damu katika wilaya ya Igunga na timu nyingine katika manispaa pamoja na halmashauri ya wilaya ya Uyui na wamelenga kuwafikia wanafunzi wa sekondari kwani upatikanaji wa kundi hilo ni rahisi katika kipindi hiki.

"Kama kanda hatujachoka kuhamasisha wananchi licha ya changamoto ya uelewa kwa jamii kuhusu uchangiaji damu,hivyo tumejipanga kuendelea kutoa elimu kwenye makundi yote ili tuweze kuwa na damu za kutosha kwenye hospitali zetu".

Hata hivyo alisema kama Kauli mbii ya kampeni hii inavyosema "changia damu,ili kuokoa maisha ya akina mama wanaoleta uhai duniani "hivyo jamii inapaswa kuelewa uchangiaji wa damu mara kwa mara ni muhimu ili kuokoa vifo vya akina mama wajawazito wanapoteza uhai wakati

wanapotimiza haki yao ya kuleta watoto duniani.

Naye Afisa Mhamashaji wa kanda hiyo Constantine Chiba alisema wamejiwekea utaratibu kutoa elimu ya kuchangia damu kwa kutembelea vijiji mbalimbali kwenye mkoaa huu,nyumba za ibada pamoja na makundio mengine katika jamii ili kuweza kuwa na akiba ya damu na pindi inapohitajika waweze kuokoa maisha ikiwemo ya akina mama wanaojifungua.

Chiba alisema yapo makundi matano ya wahitaji wa damu yakiwemo akina mama akina mama wajawazito na watoto wachanga,wahanga wa ajali,wanaohitaji tiba ya upasuaji,wenye matatizo ya kuishiwa damu (sikoseli) na kundi la mwisho ni watu wote ambao wanawenza kuugua na kuhitajika kuongezewa damu"kumbe sisi sote ni wahitaji wa damu kwani hatuyawezi kuyakwepa makundi haya yote kama binadamu kwani ugonjwa au ajali haiwezi kukwepa jinsia au umri wa mtu".



Wanafunzi wa shule za Sekondari mkoani Tabora wakichangia damu kwenye wiki ya uhamashaji damu ili kuokoa maisha ya akina mama wajawazito

Tanzania yapiga hatua utoaji huduma za afya ya mama na mtoto

NA MWANDISHI WETU

“

Kati ya vituo 192 vilivyokuwapo vituo vya afya vilikuwa 115 na hospitali za halmashauri zilikuwa 77, sasa vimeongezeka kufikia 586 kati ya hivyo hospitali za halmashauri ni 99 na vituo vya afya ni 487, hii ni sawa na ongezeko la vituo 394,” anabainisha.

HATUA kubwa imeshuhudiwa nchini Tanzania katika utoaji wa huduma za afya hususan zile za uzazi, mama na mtoto ndani ya kipindi cha miaka mitano (toka mwaka 2015/16 hadi 2020).

Uimarishwaji wa miundombinu ya kutolea huduma za afya ni mionganoni mwa hatua hizo ambapo Serikali ya Awamu ya Tano imesimamia ipasavyo eneo hilo na kwa dhati.

“Ndani ya miaka hiyo mitano jumla ya vituo 1,797 vimejengwa, kati ya hivyo Zahanati ni 1,198, vituo vya afya 487, hospitali za halmashauri 99, hospitali za mikoa 10 ikiwamo Hospitali ya Mkoa wa Mara ya Mwalimu. Nyerere Memorial Hospital.

“Hospitali hii ya Mkoa wa Mara ujenzi wake uliasisiwa na Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu J.K. Nyerere mnamo 1977, zaidi ya miaka 40 iliyopita,” anabainisha Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu.

Waziri Ummy anasema Serikali pia imejenga na kufanya upanuzi wa Hospitali tatu za Rufaa za Kanda, Hospitali ya Mtwara, Hospitali ya Bugiri (Ujenzi mpya) na upanuzi mkubwa wa Hospitali ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini - Mbeya (MZRH).

Anasema jengo hilo linalojengwa kwa ajili ya MZRH ni kubwa lenye ghorofa tano lina uwezo wa vitanda 223 maalumu kwa ajili ya huduma za mama na mtoto ikiwemo vyumba vitatu vya upasuaji.

“Tangu 1950 haijawahi kujengwa jengo la kulaza wagonjwa la namna hii,” anasitisita Waziri Ummy.

Anaonjeza “Uwekezaji huu mkubwa uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano kwenye miundombinu ya utoaji huduma za afya umeongeza vituo vya huduma za afya ngazi ya msingi vinavyotoa huduma za upasauji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni kutoa vituo 192 mwaka 2015 hadi 586 mwaka 2020.

“Kati ya vituo 192 vilivyokuwapo vituo vya afya vilikuwa 115 na hospitali za halmashauri zilikuwa 77, sasa vimeongezeka kufikia 586 kati ya hivyo hospitali za halmashauri ni 99 na vituo vya afya ni 487, hii ni sawa na ongezeko la vituo 394,” anabainisha.

WATOTO WACHANGA

Anasema Serikali imeongeza pia idadi

ya vituo vya huduma kwa ajili ya watoto wachanga wanaozaliwa wakiwa na shida ya kupumua, uzito pungufu na maambukizo ya bakteria (Neonatal Care Units) kutoka vituo 14 mwaka 2015 hadi vituo 104 mwaka 2020 sawa na ongezeko la vituo 90.

“Vituo vinavyotoa huduma ya Kangaroo (KMC) ikiwa ni njia ya kiasili ya kumtunza mtoto aliyezaliwa njiti vimeongezeka kutoka 80 mwaka 2015 hadi 104 mwaka 2020.

Anasema pia imeongeza vituo vya upimaji wa saratani ya mlango wa kizazi kutoka vituo 176 mwaka 2015 hadi kufikia 650 mwaka 2020 sawa na ongezeko la vituo 474 ambapo vimewekewa vifaa vya kisasa vya uchunguzi wa awali wa saratani hiyo pamoja na kuwajengea uwezo


damu salama ambapo vituo vitano ujenzi wake unakamilishwa,” anabainisha.

Anaonjeza “Hii ni pamoja na kujengea uwezo timu za Halmashauri 184 katika ukusanyaji wa damu kwa ajili ya kuokoa maisha ya mama na mtoto pamoja na wagonjwa wengine.

“Hivyo, upatikanaji wa damu salama kwa ajili ya akinamama na watoto kama kundi lenye uhitaji mkubwa umeongezeka kutoka chupa 196,735 mwaka 2015 hadi chupa 309,376 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 57.

AJIRA

Waziri Ummy anasema 2016 hadi 2020 jumla ya Watoa huduma za afya 14,479 wenye ujuzi walajiriwa na kufikia watumishi 100,631 mwaka 2020



watumishi.

“Ujenzi na upanuzi huu umesogezza huduma muhimu kwa ajili ya dharura ya uzazi na watoto karibu na wananchi kuitia uimarishaji wa vituo vyetu vya afya ya msingi, hivyo kuwaondolea kero na gherama kubwa walizokuwa wanazitumia kufuata huduma hizi mbali na maeneo yao na hivyo kuboresha maisha yao.

“Aidha, Serikali imeendelea kuimarisha vituo saba vya kanda vya damu salama na kuongeza vituo vidogo 14 (satellites) vya

ikilinganishwa na watumishi 86,152 mwaka 2015.

Anasema watumishi hao ni pamoja na madaktari, wauguzi na wakunga, wafamasia, watalamu wa maabara na kada nyingine ambao walipelekwa katika vituo mbalimbali vya utoaji huduma nchi nzima kulingana na mahitaji ya mikoa na wilaya na kuwesheha kuimarika kwa utoaji wa huduma za afya ikiwa ni pamoja na afya ya uzazi na mtoto.

“Ni dhahiri kuwa uwepo wa watumishi

INAENDELEA UK. 18

Tanzania yapiga hatua utoaji huduma za afya ya mama na mtoto

INATOKA UK. 17

hao umewezesha kuongezeka kwa akinamama wanaozalishwa na watoa huduma wenye ujuzi kutoka asilimia 64 mwaka 2015 hadi asilimia 80 mwaka 2020.

"Hivyo kufikia lengo la utekelezaji tulilojiweke katika mpango mkakati wa pili wa kuboresha afya ya uzazi, mama, mtoto mchanga, mtoto chini ya miaka mitano na kijana (One Plan II) wa mwaka 2016 – 2020," anasitiza.

DAWA, VIFAA TIBA & VITENDANISHI

"Tutaendelea kuimarisha upatikanaji wake kwa ajili ya huduma za afya nchini, kumekuwa na ongezeko la bajeti ya dawa kutoka shilingi bilioni 31 mwaka 2015 hadi bilioni 270 mwaka 2019/20," anasema.

Waziri Ummy anafafanua kwamba "Ongezeko hilo limewezesha kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa dawa muhimu kwa ajili ya afya ya uzazi na mtoto kutoka asilimia 53 mwaka 2015 hadi asilimia 96 Juni 2020.

"Dawa hizo ni pamoja na dawa ya kuzuia kuvuja kwa damu baada ya kujifungua aina ya Oxytocin, dawa za kudhibiti kifafa cha mimba zinazotolewa kwa sindano aina ya magnesium sulphate, dawa za kuongeza damu aina ya Fefo na pia upatikanaji wa njia za kisasa za uzazi wa mpango.

GARI ZA KUBEBEA WAGONJWA

Anasema katika kipindi cha 2015/16 hadi Juni, 2020 Serikali imendelea kuimarisha pia huduma za afya ya uzazi na mtoto kwa kununua magari ya kubebea wagonjwa (ambulance) 152 ambayo yamesambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya kwenye halmashauri mbalimbali nchini.

"Magari haya yamewezesha kuokoa maisha ya akina mama wengi pindi wanapotakiwa kufikishwa kwa haraka katika vituo vya kutolea huduma," anabainisha.

HUDUMA ZA CHANJO

Anasema ili kuimarisha upatikanaji, uhifadhi na usambazaji wa Chanjo, Serikali imendelea kutoa fedha za kununulia chanjo pamoja na ukarabati wa maghala ya kuhifadhia chanjo eneo la Mabibo Dar es Salaam.

"Imenunua magari 74 ya kubebea chanjo, ununuzi majokofu 1,385 yanayotumia nguvu za jua ambapo Magari

hayo na Majokofu yalisambazwa ngazi ya Halmashauri na Taifa," anasitiza.

Anaongeza "Kuwepo kwa majokofu haya sio tu kumeimarisha mnyororo baridi wa chanjo lakini pia kumewezesha vituo vya afya hususani zahanati na vituo vya afya kupunguza gharama za uendeshaji kwa ni awali walikuwa wanunuua mitungi ya LP gas takribani kila mwezi.

VIASHIRIA VYAIMARIKA

Waziri Ummy anabainisha "Kutokana na maboresho yaliyofanyika katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano, viashiria vikuu vya mwenendo wa huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto, vimeendelea kuimarika.

"Idadi ya wanawake wanaotumia huduma za afya ya uzazi kabla ya ujauzito na baada ya kujifungua imeongezeka kutoka asilimia 32 mwaka 2015/16 hadi asilimia 43 mwaka 2020," anasema.

Anasema kuimarisha kwa ubora wa huduma za kliniki kwa wajawazito na watoto kumeleta ongezeko kubwa la akinamama wanaohuduria mara nne au zaidi kwenye kliniki ya wajawazito kutoka akinamama 747,524 (asilimia 39) mpaka akinamama 1,758,191 (asilimia 81) Juni 2020.

"Kiwango cha wajawazito wanaojifungua kwenye vituo vya kutolea huduma kimeongezeka kutoka akinamama 1,226,707 (asilimia 64) mwaka 2015 mpaka akinamama 1,801,603 (asilimia 83) Juni 2020, tumevuka lengo la asilimia 80 tulilokuwa tumejiweke katika

Mpango Mkakati wa Afya ya Uzazi na Mtoto (2016-2020)," anasitiza.

VIFO VYAPUNGUA

"Kwa kutumia takwimu za mfumo wa kufuatilia vifo vitokanavyo na uzazi, tumeshuhudia kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi kwa zaidi ya asilimia

71 ukilinganisha na vifo viliviyotolewa taarifa kuititia utafiti mwaka 2015/2016 (TDHS).

"Hali hii inaashiria kuwa tutakopofanya utafiti wa hali ya vifo vitokanavyo na uzazi na watoto nchini ifikapo mwaka 2021, kiwango cha vifo hivyo nchini Tanzania kitakuwa chini ya vifo 190 kwa vizazi hai 100,000 ukilinganisha na vifo 556 kwa vizazi hai 100,000 kama ilivyotolewa taarifa kwenye utafiti wa mwaka 2015/16.

"Mwenendo huu unaendana na takwimu

za utafiti uliofanywa Mkoa wa Kigoma kwa Kushirikiana na Taasisi ya Thamini Uhai kwa ufadhilli wa CDC mwaka 2018 ambapo kiwango cha vifo vitokanavyo na uzazi kilikuwa ni 174 kwa kila vizazi hai 100,000," anafafanua.

Anasema taarifa za mapitio ya vifo hivi zinaonesha kuwa zaidi ya asilimia 80 ya vifo vitokanavyo na uzazi vinazuilika.

"Kwani, sababu zake ni pamoja na kupoeteza damu wakati wa uchungu, kujifungua na baada ya kujifungua na kifafa cha mimba ambavyo huchangia asilimia 50 ya vifo vyote.

"Sababu zingine ni upungufu wa damu unaotokana zaidi na lishe duni na ukosefu wa madini chuma mwilini hasa wakati wa ujauzito, maambukizi ya bakteria baada ya kujifungua, uchungu kinzani, kupasuka mfuko wa uzazi nakadhalika.

MIKAKATI MADHUBUTI

Anasema Serikali imendelea kutekeleza afua mbalimbali za kulinda afya ya mtoto ikiwa ni pamoja na utoaji wa chanjo mbalimbali, udhibiti wa magonjwa mbalimbali, Afya ya Usafi wa Mazingira na Mafunzo ya IMCI kwa watoa huduma za afya nchini.

"Itaimarisha upatikanaji wa dawa muhimu za watoto kwa zaidi ya asilimia 96, ujenzi na ukarabati wa wodi za watoto wachanga na utoaji wa elimu kwa wazazi juu ya unyonyeshaji katika kipindi cha miaka miwili kumechangia kupungua zaidi kwa vifo vya watoto nchini.

"Kwa kutumia mfumo wa ufuatiliaji wa utoaji huduma za afya unaonesha kuwa vifo vya watoto wa umri chini ya mwaka mmoja vilikuwa vifo 9 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2019/20.

"Takwimu hizi zinaonesha mafanikio makubwa ukilinganisha na Takwimu za utafiti wa Viashiria vya Afya wa mwaka 2015/16 ambapo vifo vya watoto chini ya mwaka mmoja ilikuwa vifo 43 kat i ya vizazi hai 1000

"Takwimu zetu za mwaka 2019/20 vifo vya watoto chini ya miaka mitano vilikuwa vifo 11 kat i ya vizazi hai 1,000, ambapo takwimu za utafiti wa mwaka 2015/16 ilikuwa vifo 67 kat i ya vizazi hai 1000

"Takwimu zetu za mwaka 2019/20 vifo vya watoto wachanga vilikuwa vifo 7 kat i ya vizazi hai 1,000, ambapo takwimu za utafiti wa mwaka 2015/16 ilikuwa vifo 25 kat i ya vizazi hai 1000," anabainisha.

“

Kwa kutumia
mfumo wa
ufuatiliaji wa
utoaji huduma za
afya unaonesha
kuwa vifo vya
watoto wa umri
chini ya mwaka
mmoja vilikuwa
vifo 9 kwa kila
vizazi hai 1,000
mwaka 2019/20

Siku ya Lishe Kitaifa yazinduliwa kuendeleza juhudzi za kukabili utapiamlo nchini

NA MWANDISHI WETU

Kwa mara ya kwanza, Tanzania imeadhimisha Siku ya Lishe Kitaifa Agosti 7, mwaka huu, maadhimisho ambayo yanalenga kuwaleta pamoja wananchi ili kutambua na kufahamu umuhimu wa lishe bora.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu anasema maadhimisho hayo yataendelea kufanyika miaka ijayo, yanalenga kuwa chachu ya mabadiliko katika ulaji unaofaa na mtindo bora wa maisha.

Anasema yatatumika kuhamasisha utekelezaji wa shughuli za lishe kwenye ngazi za mikoa na Halmashauri ili kutatua matatizo ya lishe yaliyopo katika maeneo yao husika.

"Yatatumika pia kuelimisha na kuhamasisha umma wa Watanzania kuhusu umuhimu wa lishe bora kwa kutumia jumbe mbalimbali, kufanya tathmini ya hali ya lishe na kutoa ushauri kwa wananchi," anasema.

Anaongeza "Serikali inatambua lishe bora ni msingi wa maendeleo ya Taifa letu, na ni moja ya eneo la kipaumbele cha kimaendeleo.

"Hivyo, kila mdau ikiwemo sekta binafsi kwa nafasi yake na wananchi kwa ujumla ana wajibu katika kupambana na aina zote za utapiamlo.

"Maadhimisho haya yalete chachu ya kujenga Taifa lenye watu wenye afya njema na ufaamu mzuri wenye uwezo wa kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za kiuchumi zikiwemo za kilimo, uvuvi, ufugaji, biashara na kazi za viwandani na maofisini," anasisitiza Waziri Ummy.

Anasema Taifa likiwa na jamii yenye lishe bora, ni dhahiri kwamba litafanikiwa kupambana na maradhi, ujinga na umaskini na hatimaye kuwa nchi ya Uchumi wa Viwanda kama ilivyodhamiriwa na Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais Dkt. John Magufuli.

Anasema kwa mwaka huu maadhimisho hayo yalipewa kauli mbiu isemayo "Mlo kamili kwenye jamii yetu unawezekana" ikilenga kuikumbusha jamii umuhimu wa kula mlo kamili katika kila mlo ili kuupatia mwili virutubishi muhimu kwa lishe na afya bora.

"Ikumbukwe kuwa mlo kamili unatokana na ulaji wa vyakula mchanganyiko kutoka katika makundi matano ya vyakula

vinavyopatikana kwenye jamii yetu," anasema.

Anaongeza "Mlo kamili unajengwa na vyakula vinavyotokana na makundi matano ya vyakula, kundi la kwanza linahusisha vyakula vyenye asili ya nafaka, mizizi na ndizi mbichi, kundi la pili linahusisha vyakula vyenye asili ya wanyama na mikunde.

"Kundi la tatu ni mboga mboga; kundi la nne ni matunda; na kundi la tano ni mafuta, sukari na asali," anabainisha.

Waziri Ummy anasema utapiamlo ni tatizo la muda mrefu na kwamba Tanzania imepiga hatua katika kupunguza viwango


kutekeleza Mpango Mkakati Jumuishi wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Afua za Lishe (National Multisectoral Nutrition Action Plan- NMNAP 2016/17-2021/22), uliozinduliwa na kuanza kutekelezwa mwaka 2016.

"Kada ya Maafisa Lishe zimeanzishwa katika Mikoa na Halmashauri zote nchini mwaka 2012 pamoja na Waratibu wa Lishe katika sekta zinazotekeliza huduma za Lishe.

"Imeanzishwa Kamati Tendaji Jumuishi ya Lishe ngazi ya Taifa inayoratibwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, pamoja na Kamati Tendaji Jumuishi za Mikoa na Halmashauri zinazosimamia masuala ya Lishe katika

“

Kiwango ambacho kitaendelea kuongezwa taratibu katika bajeti zijazo hadi kufikia kiasi cha dola 8.5 sawa na shilingi 18,000 kwa kila mtoto kama lilivyoshauri na Jopo la wataalamu wa Benki ya Dunia na wa masuala ya Afya na Uchumi Ulimwenguni...”



vya utapiamlo kwenye jamii, hususan mionganini mwa watoto wadogo, vijana balehe na akina mama walio katika umri wa kuzaa.

Anasema utafiti wa kwanza mkubwa kuhusu hali ya lishe nchini ulifanyika katika mwaka 1964 na 1967 Mikoa wa Dodoma, Kilimanjaro, Pwani na wilaya ya Karagwe, ilibainika katika asilimia 40 - 66 ya watoto waliokuwa na umri chini ya miaka mitano walikuwa na utapiamlo.

"Miaka ya karibuni Serikali imeongeza juhudzi za kupambana na tatizo la utapiamlo nchini kwa kushirikiana na wadau wetu wa Maendeleo wa ndani na nje ya nchi," anasema.

Anazitaja ni pamoja na kuandaa na

ngazi za Taifa, Mikoa na Halmashauri," anasema.

Anaongeza "Serikali kwa kushirikiana na wadau wa Lishe imeazimia na inaendelea kutekeleza afua za lishe zenyenye matokeo makubwa kama vile, utoaji wa vidonge vya Madini Chuma na Asidi ya Foliki kwa wajawazito, utoaji wa matone ya Vitamin A na dawa za minyoo na uongezaji wa virutubishi vya madini na vitamin kwenye chakula.

"Matibabu ya utapiamlo mkali kwa watoto wa chini ya miaka mitano, utoaji elimu na huduma za Lishe kwa wanawake, vijana balehe, watoto wachanga

INAENDELEA UK. 21

Siku ya Lishe Kitaifa yazinduliwa kuendeleza juhudzi za kukabili utapiamlo nchini

INATOKA UK. 20

na wadogo, elimu ya ulaji vyakula mchanganyiko na mtindo bora wa maisha kwa wanajamii wote.

"Tunafanya maboresho na kupitia sera na miongozo mbalimbali ya utekelezaji

asilimia 29 mwaka 2018.

"Pia tumeendelea kuwa na viwango vidogo vya watoto wenye ukondefu ambapo mwaka 2014 ulikuwa asilimia 4.5 na kwa uafiti wa mwaka 2018 ni asilimia 3.5," anabainisha.

Anasema hata hivyo, takwimu hizo zimeonesha bado kuna changamoto ya ongezeko la uzito uliozidi na kiribatumbo kwa wanawake walio katika umri wa kuzaa kutoka asilimia 29.7 mwaka 2014 mpaka asilimia 31.7 mwaka 2018.

"Aidha, viwango vya ulishaji wa wa vyakula vya nyongeza miongoni mwa watoto walio na umri wa miezi sita hadi 23 bado viko chini

ambapo mwaka 2018 ni asilimia 33 tuu ya watoto hao walipata vyakula vya nyongeza ipasavyo, yaani milo kutoka kwenye makundi yote yanayotakiwa na idadi ya milo inayopaswa kuliwa.

"Ni dhahiri kuwa, matatizo ya lishe nchini yanatokana na jamii kutokuzingatia ulaji unaofaa wa vyakula kutoka katika makundi hayo matano kama inavyoshauriwa na wataalaam wa lishe.

Kuhusu unyonyesaji, Waziri Ummy anasema Takwimu za Hali ya Ulishaji watoto nchini Tanzania zinaonesha takribani asilimia 97 ya watoto wenye umri chini ya miaka miwili wananyonyeshwa maziwa ya mama.

Anasema idadi ya watoto wanaoanzishiwa kunyonyeshwa maziwa ya mama kwa wakati sahihi katika kipindi kisichozidi saa moja baada ya kuzaliwa ni asilimia 53.

Anasema idadi ya watoto wanaonyonyeshwa maziwa ya mama pekee bila kupewa maji, vinywaji na vyakula vingine katika kipindi cha miezi sita ya mwanzo baada ya kuzaliwa ni

asilimia 58.

Anasema idadi ya watoto wanaoanzishiwa vyakula vya nyongeza kwa wakati sahihi katika umri wa miezi sita hadi nane ni asilimia 87.

"Idadi ya watoto wenye umri wa miezi sita hadi 23 wanaolishwa chakula kinachokidhi vigezo vya ubora kilishe ni asilimia 35. Vigezo hivyo ni idadi sahihi ya milo anayopewa mtoto kwa siku kulingana na umri wake, na mlo uwe na mchanganyiko wa vyakula kutoka kwene makundi yasiyopungua manne ya vyakula," anabainisha.

Waziri Ummy anaongeza "Sababu kubwa ya utapiamlo kwa watoto ni ulishaji usio sahihi ambao huchangiwa na majukumu mengi yanayomkabili mama na hivyo kukosa muda wa kutosha wa kumtunza mtoto.

"Ni dhahiri kuwa mchango wa mwanamke katika familia, ajira na uzalishaji kwa ujumla ni mkubwa hivyo ni muhimu kuwatia moyo na kuwasaidia wanawake ili waweze kufanya majukumu ya uzalishaji na utunzaji familia kwa ukamilifu.

Anasema "Ujumbe mahsus wa Wiki ya Unyonyesaji Duniani kwa mwaka huu 2020 ulisema "Tuwawezeshe wanawake kunyonyesha kwa afya bora na ulinzi wa mazingira" unahimiza na kukumbusha wajibu wa makundi mbalimbali ya wadau wa lishe kusaidia na kuondoa vikwazo mbalimbali vinavyochangia baadhi ya wanawake kushindwa kunyonyesha watoto wao kikamilifu.

"Kauli mbiu pia inahimiza uwajibikaji wa pamoja wa wadau ikiwemo Watumishi katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Watoa Huduma za Afya, Asasi za Kiraia, Sekta Binafsi, Waandishi wa Habari, na jamii kwa ujumla katika kulinda, kuendeleza na kusaidia unyonyesaji maziwa ya mama na hivyo kuboresha lishe ya jamii.

"Unatukumbusha kuwa kama jamii tuna wajibu wa kuwawezesha wazazi, hususani wanawake waweze kunyonyesha watoto wao maziwa ya mama pekee kwa miezi sita ya mwanzo baada ya kujifungua. Aidha watoto wanapotimiza miezi sita waanzishiwa vyakula vya nyongeza vyenye ubora kilishe huku wakiendelea kunyonyeshwa hadi watakopotimiza umri wa miaka miwili," anasisitiza Waziri Ummy.



**Waziri wa Afya,
Maendeleo ya
Jamii, Jinsia, Wazee
na Watoto Ummy
Mwalimu akiangalia
mpangilio wa chakula
wakati wa kilele
cha wili ya lishe
iliyofanyika jijini
Dodoma**

wa afua muhimu za Lishe nchini.

"Katika kuongeza kasi ya kupambana na utapiamlo nchini, Serikali ya Awamu ya Tano ilitoa Mwongozo kwenye Bajeti ya mwaka 2017/18 wa kutenga kiasi cha shilingi 1000 kwa ajili ya masuala ya lishe kwa kila mtoto wa umri chini ya miaka mitano.

"Kiwango ambacho kitaendelea kuongezwa taratibu katika bajeti zizajo hadi kufikia kiasi cha dola 8.5 sawa na shilingi 18,000 kwa kila mtoto kama liliyoshauri na Jopo la wataalamu wa Benki ya Dunia na wa masuala ya Afya na Uchumi Ulimwenguni," anasema.

Anasema kutokana na juhudzi hizmo wameshuhudia kuboreka kwa hali ya lishe kwa kutumia viashiria mbalimbali.

"Kulingana na uafiti wa hali ya lishe nchini uliyofanyika mwaka 2018, matokeo yake kuonesha, udumavu umepungua kutoka asilimia 34.4 mwaka 2014 hadi asilimia 31.8 mwaka 2018.

"Upungufu wa damu kwa wanawake walio katika umri wa kuzaa umepungua kutoka asilimia 45 mwaka 2010 mpaka